**KAMBI YA VIJANA WAKRISTO TANZANIA TAREHE: JAN, 05 HADI 10, 2015**

**Makusudi: Kujifunza moyo wa Yesu**

Utangulizi

- Mwaka 2002, kundi la wanasayansi walichapisha Picha ambayo ilikuwa inafurahisha sana.Walichukua mafuvu kutoka kwa Wayahudi kipindi cha Yesu Kristo, na kuyatumia, pamoja na vitu vingine vya kihistoria vinavyojulikana, ili kuwasilisha taswira ya namna Yesu alivyo kuwa.
- Wakati Picha hii, na hakika, sivyo hasa inavyo onekana, (walikuwa hawana kamera katika kipindi hicho, na hakuna hata mtu mmoja aliyechukua picha wakati huo ambayo tunayo mpaka leo), imekadiriwa jinsi ambavyo angeonekana.
- Taswira hii ni tofauti sana na picha nyingine nyingi za Yesu namna alivyo onekana. Watu weupe hudhani kwamba Yesu alikuwa kama wao, watu weusi vile vile, n.k. Watu hupenda kujifananisha nae kwa vile walivyo.
- Watu hupenda kufanya hivyo wakiwa na tabia na moyo wa Yesu pia. Hutengeneza picha katika akili zao kwa kile wanachokipenda, au kutoka katika mistari wanayoipenda, na kuweka mbali yale wasiyoyapenda.
- Mfano mzuri ni mwanafunzi mhubiri niliye mfahamu  chuoni ambaye alisema kwamba Yesu wake ( Yesu anayemfikiria katika mawazo yake) asinge mkataza mtu yeyote kuoa au kuolewa, bila kujali Mathayo 5:32 na Mathayo 19:9 inavyofundisha. Yesu aliyeko katika akili yake na Yesu halisi ni watu wawili tofauti.
- Kamwe tusiangukie kwenye mtego huo. Mara zote tunapaswa kuwa, watu wa kujitahidi kumfahamu Yesu hasa ni nani na kumfuata yeye. Tujifunze tabia zake zilikuwaje.
- Katika juma hili tutakwenda kujfunza tabia na moyo wa Yesu halisi.

I. Yesu alikuwa na moyo wa kutii (Siku ya kwanza 1.)
   A. Yesu alimtii Mungu kila wakati, katika yote alitenda.
      1. Yohana 6:38.
      2. Wafilipi 2:5-9.
      3. Waebrania 4:15.

   B. Tunapaswa kumtii yeye kama tunataka kujiita sisi  ni wafuasi wake.
      1. Yohana 14:15, 21-24.
      2. Yohana 15:14.
      3. 1 Yohana 2:3-6.
      4. 1 Yohana 5:2-3.
      5. Luka 6:46-48.
   C. Utii pia unalinganishwa katika mahusiano ya kifamilia na Yesu
      1. Mathayo 12:46-50.
      2. Luka 11:27-28.
   D. Je’ nipo tayari kuwa na moyo wa utii kwa Bwana?
      1. Jinsi ninavyo vaa. Kujisitiri.
         a. 1 Timotheo 2:9-10.
         b. 1 Petro 3:1-6

2. Malengo yangu/Makusudi katika maisha: Ni uinjilisti.
    a. Marko 16:15-16.
    b. Mathayo 28:18-20.
    c. 2 Wakorintho 4:3-6; 5:17-21.
3. Namna ninavyo zungumza na wengine: Usisengenye.
    a. 1 Ptro 4:15-16.
    b. 1 Wathethalonike 4:11-12.
    c. 2 Wathesalonike 3:11.
4. Ninashughulika vipi na mamlaka: Kutii mamlaka.
    a. Warumi 13:1-7.
    b. 1 Petro 2:13-17.

.

II. Yesu alikuwa na Moyo wa uaminifu na uwajibikaji. (Siku ya 2.)

A. Yesu alijitoa yeye mwenyewe kwenye mapenzi na mpango wa Mungu. Luka 22:39-44.
    1. Hata kufikia kutoa jasho la damu kwa uchungu na msongo wa hisia.
    2. Hakutaka kufa, lakini ilimpasa kufanya hivyo kwa sababu ilikuwa ni mpango na mapenzi ya Mungu.

B. Neno "kujitoa" katika Agano Jipya linabeba maana ya "kutoa badala ya" au "kudhamini" tazama pia Luka 23:46, "mikononi mwako naiweka roho yangu".

C. Makusudi ya Yesu ni kufanya mapenzi ya Mungu, bila kujali chochote.
    1. Yohana 5:30.
    2. Yohana 6:38.

D. Je' nitayatoa maisha yangu yote na moyo wangu wote kufanya mapenzi ya Mungu katika maisha yangu"? Nitatoa kila sehemu ya maisha yangu kwa mapenzi yake na mpango wake?
    1. Namna ninavyo muabudu Mungu: katika roho na kweli, kufuata amri zake katika uongozi, "kwa unyofu na utaratibu" n,k.
        a. Yohana 4:24.
        b. 1 Wakorintho 14:34-35,40.
        c. 1 Timotheo 2:11-14.
    2. Kufanya mambo katika kanisa, na katika ibada, Namna Mungu anavyotaka (hii ni kwa mamlaka yake): Wakolosai 3:17.
    3. Kusimama kwa ajili ya kweli, hata kama sio kawaida.
        a. Waefeso 6:11-18.
        b. Mathayo 10:32-33.
        c. Luka 12:8-9.
    4. Fanya kazi kwa Mungu kama kusudi lako la kwanza katika maisha yako: 1 Wakorintho 15:58.

III. Yesu alikuwa na moyo wa Msamaha na Huruma (Siku ya 3)

A. Yesu, hata akiwa katika maumivu makali, alikuwa na moyo wa msamaha. Luka 23:34.

B. Kusudi zima la Yesu kuja ulimwenguni ni msamaha wa dhambi.
    1. Luka 19:10.
    2. Mathayo 20:28.

3. Warumi 1:16.
4. 1 wakorintho 15:1-4.

C. Moyo wa Mungu mara zote kwetu umekuwa kwa ajili ya toba na msamaha.
1. Isaya 38:17.
2. Mika 7:18-19.
3. Yeremia 31:34.
4. Isaya 43:25.
5. Zaburi 103:8-14.

D. Tumeamriwa kuwa watu wa kusamehe.
1. Mathayo 6:14-15.
2. Marko 11:24-25.
3. Luka 17:3-4.

E. Msamaha wetu ni kutambua kuwa hauma mpaka. Mathayo 18:21-22.

F. Msamaha wetu ni kwa sababu sisi tumesamehewa sana.
1. Mathayo 18:23-35.
2. Wakolosai 3:13.
3. Waefeso 4:32.

G. Kuna tofautu kati ya “nisamehe” na “pole”.
1. “Pole” ina maana kwamba “ kosa” halikuwa la makusudi na halikuwa kubwa na kuna sababu nzuri iliyosababisha kosa kutendeka. Kwa mfano: umemkanyaga mtu mguuni na unasema “nisamehe.” Na unamanisha “Pole” kwa sababu hukukusudia kufanya hivyo, na sio kosa baya sana hata hivyo.
2. “Nisamehe” katika hali yakurudisha uaminifu tena ambapo jambo baya, limekusudiwa, na hapa linasamehewa. Hatumuambii Mungu “Pole” kwa makosa ya dhambi zetu, kwa sababu hakuna bahati mbaya katika dhambi. Tunamuomba Mungu atusamehe. Hatuna udhuru wowote wakusema tunapo danganya au kutamani au kuwachukia wengine tupo sawa. Tunataka Mungu atusamehe. Hivyo ni LAZIMA tuwasamehe wale wanaotukosea. Bila kujitetea kwao, kwasababu kile walichokifanya sio kibaya hata hivyo, lakini tuwasamehe, kuangalia walichokifanya na kukubali kuwa ni kibaya (labda kibaya sana), bali tuwasamehe bila kujali.

IV. Yesu alikuwa na Moyo wa kuwafanya watu wabadilike. (Siku ya 4).

A. Yesu alisisitiza mabadiliko ya mioyo ya watu waliomfuata yeye.
Maisha yao yaliyopita hayajalishi (mara nyingi alihusika na wenye dhambi ), lakini mabadiliko yalipaswa kufanyika.
1. Marko 10:17-23. Kijana tajiri.
2. Yohana 6:66-67. Makutano.

B. Ametuambia kwamba tutubu, sivyo tutaangamia. Luka 13:3.

C. Toba inamaana kugeuka nakuacha kufanya uovu.
1. Mathayo 12:41.
2. Yohana 3:10.

D. Tunapaswa kuhubiri Toba kama sehemu ya Injili.
1. Luka 24:46-47.
2. Matendo ya Mitume 2:38-39.

E. Tunapaswa kuweka msisitizo wa roho ya toba katika maisha yetu yote ya ukristo. 1 Yohana 1:5-10.

F. Hatupaswi kujiona kuwa sisi ni bora kuliko wengine kwasababu hata sisi tunapambana na dhambi zinazo wasumbua.
    1. Luka 18:9-14.
    2. Yakobo 1:12-15. Tunajaribiwa kwa tamaa zetu wenyewe
G. Tunapaswa kutoka katika ile dhambi inayotuzunguka.
    1. Wagalatia 5:19-21.
    2. 1 Wakorintho 6:9-11.
H. Wale wanaong’ang’ania dhambi hawataingia Mbinguni.
    1. Ufunuo 20:11-15.
    2. Ufunuo 21:8.

Je’ nikweli tunataka kuwa na roho na tabia na moyo wa Yesu aliokua nao? Bwana atusaidie kuendeleza mambo haya katika tabia zetu wenyewe.